**Ripoti ya Mwaka 2006 inatoa muhtasari wa takwimu za hivi karibuni kuhusu maendeleo kufikia malengo ya MKUKUTA ya kupunguza umaskini Tanzania.**

Maeneo makuu yanayoelezwa katika ripoti hii ni pamoja na:

Kundi I: Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato
Kundi II: Kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii
Kundi III: Utawala bora na uwajibikaji

Ripoti hii inatolewa na Kamati ya Utafiti na Uchambuzi, chini ya Mfumo wa Usimamizi wa MKUKUTA, katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.



ISBN: 9987-615-10-4

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## MKUKUTA

### MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI TANZANIA

# RIPOTI YA MWAKA 2006:

## Maendeleo ya kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na utawala bora Tanzania

Desemba 2006



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MKUKUTA

### MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI TANZANIA

# RIPOTI YA MWAKA 2006:

## Maendeleo ya kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na utawala bora Tanzania

Kundi la Utafiti na Uchambuzi, Mfumo wa Usimamizi wa MKUKUTA,
Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

Desemba 2006

**Maelezo zaidi na nakala za taarifa hii hupatikana:**

Sekretariat ya MKUKUTA, Kitengo cha Kupunguza Umaskini,
Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji,
S.L.P. 9242, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2113856/2124107
Barua pepe: secretariat@povertymonitoring.go.tz
Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz

**Kutoka Sekretariat ya Kamati ya Utafiti na Uchambuzi:**

Research on Poverty Alleviation (REPOA)
Kitalu 157, Mtaa wa Mgombani, Regent Estate,
S.L.P. 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2700083/0784 555 655
Barua pepe: repoa@repoa.or.tz
Tovuti: www.repoa.or.tz

Usanifu: Creative Eye Ltd.
Michoro: Abdul Gugu

© Kamati ya Utafiti na Uchambuzi, 2007

ISBN: 9987-615-10-4

# Yaliyomo


**Shukrani** v
**Utangulizi** vi

**SEHEMU YA I: Malengo makuu na namna ya kupima mafanikio**

MKUKUTA ni nini? 1
Nani anahusika kwenye MKUKUTA? 1
Ni nini malengo makuu ya MKUKUTA? 2
Kwanini makundi haya matatu ya MKUKUTA yalichaguliwa? 2
Je kuna kundi moja la MKUKUTA muhimu zaidi ya mengine? 6
Maendeleo kufikia malengo ya MKUKUTA yatapimwa vipi? 7
Mfano wa jinsi maendeleo ya MKUKUTA yanavyopimwa 8
Ni takwimu gani zinatumika? 9
Namna ya kutafsiri takwimu 9

**SEHEMU YA II: Ni mafanikio gani yalipatikana wakati wa mwaka wa kwanza wa MKUKUTA**

**Kundi la I: Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato** 11

- Lengo 1: Usimamizi mzuri wa uchumi 15
- Lengo 2: Ukuaji wa uchumi endelevu na mpana 16
- Lengo 3: Hifadhi ya chakula 17
- Lengo 4 na 5: Kupunguza umaskini wa kipato vijijini na mijini 18
- Lengo 6: Nishati ya kuaminika na ya gharama nafuu 19

**Kundi la II: Kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii** 20

- Lengo 1: Elimu 21
- Lengo 2: Afya 23
- Lengo 3: Maji safi na salama, usafi unaofaa, makazi mazuri na uhifadhi wa mazingira 26
- Lengo 4: Kulinda makundi maalum na wasiojiweza 28
- Lengo 5: Huduma za jamii kwa wote 29

**Kundi la III: Utawala bora na uwajibikaji** 30


- Lengo 1: Utawala na utawala wa sheria 32
- Lengo 2: Mgawanyo sawa wa rasilimali za umma na kupungua kwa rushwa 33
- Lengo 3: Utumishi wa umma wenye ufanisi 35
- Lengo 4: Haki za masikini na wenye mahitaji maalum katika mfumo wa sheria 36
- Lengo 5: Kupunguza kutengwa kisiasa na kijamii na kutovumiliana 37
- Lengo 6: Kuboresha usalama, kupunguza uhalifu na kuondoa unyanyasaji wa kijinsia na ukatili majumbani 37
- Lengo 7: Kudumisha utambulisho wa kiutamaduni wa Taifa 37

**Muhtasari wa maendeleo ya MKUKUTA ya mwaka 2006** 38

## SEHEMU YA III: Wewe na MKUKUTA

**Je, wewe unaweza kufanya nini?** 39
**Usambazaji wa habari muhimu** 40
**Marejeo** 41
**Vifupisho** 42

Mwongozo huu umetolewa kwa lugha nyepesi kwa ajili ya wananchi wa kawaida. Lengo ni kuyafanya masuala yaliyomo katika ripoti ya mwaka 2006 kuhusu maendeleo ya kufikia malengo ya MKUKUTA yaeleweke kwa idadi kubwa ya watu wa kawaida na kuwahamasisha kuwa washiriki wazuri katika mchakato mzima. Ukitaka kujifunza au kujua zaidi kuhusu MKUKUTA, malengo yake na viashiria, ama maendeleo na hatua zilizofikiwa, tafadhali angalia ripoti kamili inayopatikana katika lugha ya kiingereza iitwayo "Status Report 2006: Progress towards the goals for growth, social well-being and governance in Tanzania".



# Shukrani

Mipango ya uandaaji wa ripoti hii (Status Report 2006), haikuwa rahisi na ilihusisha watu na taasisi mbalimbali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, aliweka mazingira mazuri yaliyowezesha serikali kwa upande mmoja, na taasisi za utafiti kwa upande mwingine kushirikiana kukamilisha ripoti hii.

Ripoti hii imeandaliwa na Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi, wa Mwenendo wa Kufuatilia Utekelezaji wa MKUKUTA. Taarifa za msingi zilikusanywa katika kipindi cha miezi kumi na mbili kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serekali, pamoja na taarifa mbali mbali za ki-utafiti, na kutoka katika vyombo vya habari. Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi, pia iliwapa kazi ya kuandaa taarifa za awali za kitaalamu kwa makundi ya MKUKUTA ambazo zilifanywa na Dkt. J. Kweka wa ESRF, K. Dyer wa Maarifa ni Ufunguo na Prof. S. Wangwe wa Daima Associates. Taarifa hizi zilipitiwa na wajumbe wa Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi.

Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Ofisi ya Takwimu na Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi, waliratibu zoezi zima. L. Msongole na Prof. J. Semboja walifanya kazi ya kuhakiki ripoti nzima na kuhakikisha usahihi wa uchambuzi. Shukrani pia ziwaendee watendaji wa REPOA kwa kazi yao nzuri wakiwa Sekretariati iliyoshughulikia uandaaji wa ripoti.

Watu wengine waliochangia kufanikisha ripoti hii ni pamoja na kundi lililohusika na ukusanyaji wa taarifa wakiwemo J. Mwangi, D. Sango, B. Mwanaidi, na D. Mwita. Wapitiaji wa ripoti hii kutoka RAWG walikuwa M. Kamugisha, Dr. J. Kipokola, Dr. F. Njau, H. Raha, M. Mcha, R. Tukai, A. Makbel, J. Biswaro, J. Mahon, V. Leach na A. Albee. Mwisho, C. Daly alifanya kazi ya kuiandika ripoti hii upya katika lugha rahisi, na D. Rweyemamu, aliipitia na kuihariri tafsiri ya Kiswahili ya toleo hili la lugha rahisi.

# Utangulizi

Karibu kwenye ripoti ya hali ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania ya mwaka 2006: Maendeleo ya kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na utawala bora Tanzania.

Jina langu ni Babu; nitakuongoza katika kupitia vipengele mbalimbali vya ripoti hii pia nitakusaidia kufafanua baadhi ya maneno ya kitaalamu yaliyotumika kwenye MKUKUTA.

Katika sehemu ya kwanza nitakueleza malengo ya MKUKUTA, utekelezaji wake na namna ya kupima mafanikio yaliyofikiwa katika mwaka mmoja.



Sehemu ya

# I Malengo makuu na namna ya kupima mafanikio

## MKUKUTA ni nini?

MKUKUTA ni kifupi cha

**M**kakati wa **K**ukuza **U**chumi na **K**upunguza **U**maskini **TA**nzania.

Huu ni mkakati wa kitaifa wa miaka mitano unaolenga kuchochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kupunguza umaskini kwa Watanzania hususan wa hali ya chini.

Ofisi ya makamu wa Rais ilikamilisha maandalizi ya MKUKUTA mwezi Juni 2005 baada ya kufanya mashauriano ya kitaifa yaliyohusisha viongozi wa serikali, wahisani, wabia wa maendeleo, asasi za kiraia, wafanya biashara na wananchi kwa ujumla. Mwaka wa fedha 2005/2006 ndiyo ulikuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji rasmi wa MKUKUTA. Utekelezaji unatarajiwa kuendelea hadi mwaka wa fedha 2009/2010.

MKUKUTA unashirikisha ngazi zote za kiserikali Tanzania

- Rais na Baraza la Mawaziri
- Bunge
- Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, na,
- Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa (TAMISEMI)

Viongozi wa serikali kuanzia ngazi za vitongoji hadi serikali kuu wanafanya kazi kwa pamoja na wananchi na wadau wengine wa maendeleo kama vile:

- Wahisani na wabia wa maendeleo wa kimataifa
- Vyama vya wafanyakazi na vyama vya ushirika
- Asasi za kiraia
- Asasi za kidini
- Vyombo vya habari
- Sekta binafsi

## Ni nini malengo makuu ya MKUKUTA?

**Kama kifupi chake kinavyosema, MKUKUTA unalenga Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania.**

Hakika hili ni jukumu zito na vitu vingi vitachangia katika kufikia mafanikio. Ili kuoanisha jitihada katika ngazi zote za kiserikali, kijamii, na mashirika ya maendeleo; serikali imechagua makundi matatu ya malengo ya maendeleo ambayo inataka kuyafikia. Makundi hayo ni:

- **Kundi I:** Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato
- **Kundi II:** Kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii
- **Kundi III:** Utawala bora na uwajibikaji

## Kwanini makundi haya matatu ya MKUKUTA yalichaguliwa?

### KUNDI I: Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato

Kipato kinahusiana kwa karibu sana na ukuaji wa uchumi wa nchi lakini vikwazo kama vile ukosefu wa stadi na utaalamu, vitendea kazi, pamoja na fedha vinaweza kuathiri ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma za jamii. Hatimaye, kipato, akiba na tija vinaweza vikabaki kuwa chini.

Licha ya kujituma kwa bidii, watu binafsi na jamii kwa ujumla wanaweza wakajikuta wamekwama katika lindi la umaskini kama hakutakuwepo fursa mpya za maendeleo. Tazama kielelezo 1.




MKUKUTA unalenga kukuza uchumi wa Tanzania na kutoa mchango zaidi katika kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania wote.

Vilevile, MKUKUTA unalenga kuitoa jamii kwenye lindi la umaskini na katika kila sehemu kuweza kuondoa neno 'm/ndogo' kama ilivyoanishwa kwenye kielelezo namba moja na badala yake kuweka neno 'm/kubwa'.

Kwa maana hiyo basi, kielelezo kitasomeka kama ifuatavyo:
Kipato kikubwa ▸ Akiba kubwa ▸ Tija kubwa ▸ Kipato kikubwa kwa Watanzania wote.

Kielelezo 1: Kujinasua na Umaskini




*Chanzo: Benki ya Maendeleo ya Asia 2005*

**Kukua kwa uchumi kuna maana gani?**

Kukua kwa uchumi ni ongezeko la uwezo wa nchi kukidhi mahitaji ya watu wake kwa muda fulani. MKUKUTA unalenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kwamba ukuaji huu unawanufaisha watu wote na unakuwa endelevu.



## KUNDI II: Kuboresha hali ya maisha bora na ustawi wa jamii

Kama ukuaji wa uchumi pamoja na kipato cha wananchi vitaendelea kuwa vya chini, kunaweza kuathiri vibaya upatikanaji wa huduma za jamii na uwezo wa wananchi kuzilipia. Huduma hizi ni kama vile shule kwa ajili ya elimu bora, afya na maji.

Umaskini pia husababishwa na mgawanyo usio sawa wa rasilimali na fursa. Kwa mfano, fursa za ajira ni chache. Vipato ni vya chini, rasilimali ni chache kwa elimu na afya, na umasikini umekithiri zaidi vijijini kuliko mijini.

Pia kuna tofauti kubwa za viwango vya umaskini baina ya mikoa na wilaya zinazotokana na tofauti za maliasili, hali ya hewa, miundombinu kama vile barabara, shule na hospitali.

Kundi la II la malengo ya MKUKUTA linalenga kuboresha maisha na ustawi wa jamii kwa Watanzania wote, hususan wale maskini zaidi na makundi yenye mahitaji maalum kama vile wananchi wa vijijini, wanawake na watoto, wazee, wagonjwa na walemavu. Pia linalenga kupunguza tofauti za fursa na matokeo yake kwenye elimu, afya, na lishe katika maeneo tofauti, pamoja na kupunguza tofauti za kipato, umri, na jinsia baina ya watu mbalimbali.

MKUKUTA unatambua kwamba kuboresha maisha ya watu kuna maanisha kwamba watu wote katika jamii yetu – wanaume na wanawake, wazee na vijana, matajiri na maskini, wana fursa sawa kushiriki katika uzalishaji.

Kwa hiyo basi, MKUKUTA unafanya kazi kufikia ukuaji wa uchumi ambao ni:

- **Mpana na wa haki**
- **Endelevu**

MKUKUTA unalenga pia kutambua fursa mpya za uwekezaji katika mikoa na wilaya maskini zaidi, na pia kwa kupitia mgawanyo wa bajeti ya nchi kuboresha miundombinu na huduma za jamii katika maeneo yenye mahitaji zaidi.

## KUNDI III: Utawala bora na uwajibikaji

Ukuaji wa uchumi, kupungua kwa umaskini na kuongezeka kwa ubora wa maisha yote yanategemea matumizi mazuri, ya haki na uwazi ya rasilimali ya Tanzania.

Kwa hivyo, mafanikio ya kundi I na II ya MKUKUTA yanatengemea utimilifu wa malengo ya kundi la III la MKUKUTA – utawala bora na uwajibikaji.



**Ukuaji mpana na wa haki? Endelevu? Maneno haya yana maana gani kwa MKUKUTA na kwa Tanzania?**

**Ukuaji mpana na wa haki** unamaanisha ukuaji wa sekta zote za uchumi na kwa mikoa yote ya Tanzania. Ni ukuaji unaopanua fursa na mafanikio kwa Watanzania wengi iwezekanavyo. Sekta muhimu ya lengo hii ni kuhakikisha ya kwamba huduma za jamii zinawafikia watu wote Tanzania bila ubaguzi.

**Ukuaji endelevu au maendeleo endelevu** ni maendeleo yanayokidhi mahitaji ya kizazi cha sasa bila kuathiri yale ya vizazi vijavyo. Kwa mfano MKUKUTA unalenga kufikia ukuaji usioharibu mazingira wala kufilisi maliasili yetu kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

Haki za binadamu, mfumo wa haki unaofanya kazi na mapambano dhidi ya rushwa ni vipengele muhimu vya kundi la III. Pia MKUKUTA unatambua kwamba uwezo wa kupata habari za serikali na ushiriki mpana wa asasi za kiraia katika kutengeneza, kutekeleza na kusimamia sera ni muhimu kwa utawala bora.

Ushiriki wako katika mabadiliko ya serikali za mitaa, kamati za shule, ushrika, vyama vya wakulima, na katika juhudi zingine za maendeleo ya jamii yako utasaidia mifumo ya serikali kuwa ya kidemokrasia zaidi, ya kishirikishi, na inayowajibika zaidi.

Serikali inahitaji kusikia sauti ya Watanzania wote, ikiwemo yako ili kufanikisha MKUKUTA. MKUKUTA unatafuta hasa sauti za watu maskini na makundi maalumu ya jamii Tanzania zisikike katika maamuzi ya ngazi za juu.

**Utawala ni nini?**

Watu wengi hufikiria kwamba '**utawala**' ni sawa na 'serikali'. Hii sio sawa. Utawala ni kanuni, namna na vitendo ambavyo shirika lolote – biashara, jumiya za kiraia, kitengo cha serikali, chama cha siasa, vyama vya wakulima ama kundi lingine lolote – huvitumia kutengeneza na kutekeleza maumuzi na sera.

Katika suala la MKUKUTA, utawala unamaanisha mfumo wa sheria, namna na vitendo ambavyo ngazi zote za serikali ya Tanzania hivufuata kuendesha mambo ya taifa, rasilimali ya Tanzania, na kulinda haki na ustawi wa wananchi.

**Utawala bora** unamaanisha kwamba majukumu yote yanatekelezwa bila matumizi mabaya ya mamlaka au rushwa, kwa kuheshimu haki na sheria; yaani bila upendeleo na ubaguzi na kwa uadilifu. Kwa mfano, kodi kwa biashara zote na watu binafsi zinafaa kutozwa na serikali bila kupendelea na kwa uadilifu kulingana na sheria za nchi za kodi. Wafanyakazi wa serikali wanapaswa kutoza kiasi kinachotstahili tu kwa huduma wanazotoa.




## Je kuna kundi moja la MKUKUTA muhimu zaidi ya vingine?

Vikundi vyote vina umuhimu sawa. Kwa kweli, malengo makuu ya MKUKUTA yana husiana - hii ina maana, kukamilisha malengo ya kundi moja kutasaidia kutimiza malengo ya vikundi vingine.

Ukuaji mpana, wa haki na endelevu katika uchumi huleta mapato ya kaya makubwa, kwa kaya hivyo kupunguza kiwango cha umaskini. Mapato makubwa ndiyo huwezesha kaya na jamii kuendeleza ustawi wao kwa kuwawezesha kuwekeza fedha zao kwa lishe bora, makazi, afya, na elimu.

Utawala bora huleta mazingira ya siasa jamii yaliyo na usawa na haki yatakayowezesha ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na kupunguza umaskini. (Tazama kielelezo 2.)

**Kielelezo 2: Uhusiano kati ya malengo makuu ya MKUKUTA**




*Chanzo: "Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania", Ofisi ya Makamu wa Rais, Juni 2005.*

## Maendeleo kufikia malengo ya MKUKUTA yatapimwa vipi?

Mafanikio ya MKUKUTA yatapimwa kulingana na matokeo au malengo yaliochaguliwa. Kwa kila lengo katika MKUKUTA, viashiria vinavyohusika vimetumiwa kuonyesha kama Tanzania inakaribia, au inakwenda mbali, na malengo haya.

Kwa kuwa malengo mengi ya MKUKUTA yanahitaji mambo mengi kufanya kazi kwa pamoja ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini, mafanikio ya lengo moja yanaweza kupimwa kwa kutumia viashiria mbali mbali. Kwa makakati mzima, viashiria zaidi ya 80 vimetumika. Hivyo, kwa kila kiashiria serikali imeweka au inaweka, shabaha inazotaka kufikia mwisho wa MKUKUTA 2010. Angalia mfano ukurasa unaofuata.

Viashiria hivi vilibuniwa na kitengo cha kuondoa umaskini cha Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa kukishirikiana na wizara zingine za serikali, vitengo na mawakala; na kwa mashauriano na wawakilishi wa wabia wao wa maendeleo, asasi za kiraia na taasisi zingine za taifa.

Ripoti hii na ripoti zote zijazo za MKUKUTA zitawajulisha maendeleo ya mkakati kutokana na viashiria vya malengo ya MKUKUTA, na malengo maalum 18. Hii itamaanisha kwamba taarifa za maendeleo ya MKUKUTA zitatolewa kila mara (na zitaweza kulinganishwa) katika hiyo miaka mitano ya utekelezaji wake.

Kwa mantiki hii, itakuwa rahisi kuona kama malengo ya MKUKUTA yanatimizwa, na kama bado, ni wapi kutakapoongezwa juhudi. Kama ambavyo mafanikio ya mwaka ya MKUKUTA yatakuwa kama msingi huu wa mwaka ujao, ripoti ya mwaka 2006 itakuwa msingi mzuri wa ripoti ya MKUKUTA ya mwaka 2007.




**Kiashiria ni nini?**

**Kiashiria** kinaweza chukuliwa kama kibao cha kinachoelekeza njia ya kupita kwenda sehemu fulani na kipimo cha umbali wa safari iliyobaki. Kwa mfano, unapotembea au kupanda basi kutoka nyumbani hadi kazini, unaona vibao njiani – alama tofauti ama majumba ama vituo vya mabasi – ambavyo hukuwezesha kufahamu unapokwenda. Hivyo hivyo mafamkio kuelekea malengo ya MKUKUTA hupimwa kwa vibao maalum vilivyo njiani, ambavyo huitwa viashiria.

## Mfano wa jinsi maendeleo ya MKUKUTA yanavyopimwa

Ili tuone ni jinsi gani maendeleo ya MKUKUTA yanapimwa, hebu tuangalie kwa undani lengo moja muhimu la MKUKUTA katika kundi la 2:

### Lengo 1: Upatikanaji wa haki wa elimu bora kwa watoto wote Tanzania

Kwa kuwa mambo mengi lazima yawepo ili kutimiza lengo hili, basi viashiria kadhaa vinahitajika kuonyesha kwamba watoto wengi Tanzania wanasoma na kwamba elimu ni bora. Viashiria viwili vilivyochaguliwa kupima maendeleo ya kufikia malengo haya ni:


**Kiashiria 1:** **Jumla ya watoto wa kiume na wa kike walioandikishwa katika shule za msingi na za sekondari, wakiwamo walemavu, yatima na watoto wengine wenye mahitaji maalum.**
**NA**
**Kiashiria 2:** **Jumla ya walimu walio na ujuzi katika shule za Tanzania**

Pamoja na haya, serikali imeweka (ama iko katika hatua ya kuweka) shabaha kwa kila kiashiria kuonyesha matokeo kwa malengo yaliyokusudiwa ifikapo mwisho wa utekelezaji wa MKUKUTA mwaka wa 2009/2010. Kwa kiashiria cha kwanza hapo juu, serikali imeweka shabaha mbili.

**Shabaha 1:** **Asilimia 99 ya watoto wadogo wanaandikishwa katika shule za msingi**
**NA**
**Shabaha 2:** **Asilimia 50 ya watoto wanaandikishwa katika shule za sekondari**

**Je, MKUKUTA utafikia shabaha hizi?**

Kiasi cha kujiandikisha kilikuwa asilimia 96 mwaka wa 2006, kwa hiyo tuko karibu kufikia lengo hili. Lakini ni asilimia 13 tu ya watoto ndiyo wameandikishwa katika shule za sekondari. Kazi kubwa inahitajika ili kufikia lengo la MKUKUTA la asilimia 50 ifikapo mwaka wa 2010.



## Ni takwimu gani zinatumika?

Ripoti hii inahusisha takwimu za hivi karibuni. Kwa kadri iwezekanavyo,takwimu za kila mwaka hutolewa, lakini tafiti kubwa kama vile: Taarifa Kuu ya Sensa ya Watu na Makazi, Utafiti wa Bajeti ya Kaya (HBS), na Utafiti kuhusu Afya na Demografia Tanzania (THDS) – hazifanywi mara kwa mara. Hivyo, kwa viashiria vingine, takwimu mpya hazikupatikana kwa mwaka 2006. Takwimu mpya zitajumuishwa katika ripoti za MKUKUTA mara tafiti zitakapokamilika.

Viashiria vingine – kama usalama wa jamii na utawala – vinatumika kwa mara ya kwanza kwenye MKUKUTA. Kwa hivyo, taarifa iliyoko mwaka huu ni kidogo, ila itaongezeka jinsi mkakati unavyokua.

## Namna ya kutafsiri takwimu

Ili kupima maendeleo ya kiashiria chochote, mahali pa kuanzia lazima pachaguliwe. Kutokea hapo mabadiliko yoyota yatakayotokea – mazuri au mabaya yatapimwa mahali hapo pa kuanzia panaitwa msingi.

Kwa viashiria vingi, MKUKUTA hutumia misingi kutoka miaka 1999, 2000 au 2001. Kwa hadri takwimu mpya zinavyopatikana, zitaweza kulinganishwa na misingi hii (na takwimu zilizoko za miaka mingine) ili tuone kama takwimu hizi zinaonyesha hali bora, hali ya kutobadilika au hali mbaya.

Kisha, kutoka mwaka hadi mwaka kiashiria kinaweza kwenda juu, au chini, au kubaki pale pale iwapo kuwa mabadiliko kidogo ama bila mabadiliko. Kwa mfano, MKUKUTA unalenga kupunguza umaskini Tanzania kila mwaka na kuhakikisha kuwa haupandi tena. Mpangilo wa mabadiliko au mwelekeo fulani wa kiashiria chochote huitwa mwenendo.

Ni muhimu kujua kwamba mwenendo unaoelekea juu siyo kila mara huwa mzuri, na mwenendo unaolekea chini siyo kila mara huwa mbaya. Tathmini ya mwenendo wowote hutegemea kiashiria kimoja kimoja.

Utaona misingi ya MKUKUTA kuhusu elimu, afya na maji salama katika jedwali ya 3, 4 na 5 baadaye katika ripoti.



Kwa mfano, mwenendo unaoelekea juu katika mfumuko wa bei humaanisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma, ambalo si jambo zuri kwa kaya Tanzania. Kinyume na hili, mwenendo unaoelekea chini katika kiasi cha riba kinachotozwa na benki huonyesha kwamba kukopa fedha kunakuwa rahisi, ambalo ni jambo zuri kwa Watanzania wanaotaka mikopo.

Zaidi ya hayo, takwimu zilizotangazwa ni za jumla au wastani kwa nchi nzima. Hivyo, zinaweza kutoonyesha mambo yanayofanyika katika jamii yako. Hii ndiyo maana ni muhimu kwa viongozi wa serikali za mitaa Tanzania kufanya juhudi kukusanya na kuripoti takwimu sahihi zitokazo kwa jamii zao.

Sehemu zilizo na rangi katika jedwali za sehemu ya II (tazama jedwali 2, 3 na 4) zitakusaidia kuelewa mwenendo wa kila kiashiria na kama MKUKUTA unapiga hatua kufikia malengo yake.



Sasa twende katika sehemu ya pili ya ripoti hii, ambapo utagundua ni nini MKUKUTA umetimiza mwaka huu.



Sehemu ya

# II Ni mafanikio gani yaliyopatikana wakati wa mwaka wa kwanza wa MKUKUTA?

Karibu katika sehemu ya II ya ripoti ya hali ya MKUKUTA 2006. Katika sehemu hii, taarifa zitatolewa za hatua na maendeleo yaliofikiwa nchini mnamo mwaka wa kwanza wa MKUKUTA. Majadiliano yatatokana na malengo ya vikundi vitatu vya MKUKUTA ambavyo vimetajwa katika sehemu ya I.



## KUNDI I: Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato

**Mafanikio yaliyopatikana kutoka kundi I hupimwa kulingana na:**

A. Viashiria vya jumla, pamoja na Pato la Taifa, na
B. Viashiria vya kila moja ya malengo sita yaliyomo katika kila kundi.

### A. Pato la Taifa (GDP)

Kwa jumla, takwimu za miaka kumi iliyopita zinaonyesha kuwa uchumi wa Tanzania umekua. Kwa mfano, mwaka wa 2005, uchumi wa Tanzania ulikua kwa karibu asilimia 7.

Utaona pia katika kielelezo 3 kwamba uchumi wa Tanzania hivi karibuni umeongezeka sana hasa katika sekta za madini na viwanda. Hata hivyo, ukuaji katika kilimo umekua asilimia 5 kwa miaka michache iliyopita, na inatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.8 katika mwaka 2006 kwa sababu ya hali ya ukame uliojitokeza katika sehemu nyingi nchini.

Kilimo bado ndiyo kinachukua sehemu kubwa ya uchumi, na ndiyo kiini cha chakula na mali ghafi kwa viwanda. Kinachangia asilimia 45 ya Pato la Taifa, na karibu asilimia 60 ya mapato ya biashara za nje kwa miaka zaidi ya mitatu iliyopita. Muhimu zaidi, Watanzania wanne kati ya watano hutegemea kilimo kwa mahitaji yao yote. Kwa hivyo, inaeleweka vizuri kwamba vitega uchumi na ukuaji wa kilimo ni lazima uongezeke ili umasikini Tanzania upungue.


### Je, Pato la Taifa ni nini?

Pato la Taifa (kwa ufupi GDP) ni thamani yote ya soko la bidhaa na huduma zinazotengenezwa na nchi katika mwaka wowote. Pato la Taifa ni jumla ya thamani ya uchumi wa nchi wa mwaka mzima.

Kiasi cha mabadiliko katika Pato la Taifa kwa mwaka moja ni kipimo cha kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi. Ili kuwezesha ulinganifu wenye maana wa ukuaji wa uchumi kwa miaka tofauti, MKUKUTA hutoa ripoti ya ukuaji wa Pato la Taifa ambalo ni ukuaji wa uchumi wa Tanzania uliorekebishwa kulingana na mfumuko wa bei. Nitawaeleza mengi kuhusu mfumuko wa bei baadaye kidogo katika sehemu hii.



**Kielelezo 3: Ukuaji wa Pato la Taifa Tanzania 1996-2005 kulingana na sekta**




*Chanzo: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tafiti za Kiuchumi, miaka mingi*

Matumizi ya fedha za serikali ili kuwezesha ukuaji uwe wa haraka – kama vile kuwekeza katika barabara, afya na elimu – ni lazima. Pia, kutengenezwa kwa mpango maalum wa ukuaji utasaidia kuvipa kipaumbele vitega uchumi muhimu Tanzania – kwa sekta binafsi na serikali. Mpango wa ukuaji wenye mwelekeo pamoja na uongozi mzuri wa uchumi utasaidia kuhakikisha vitega uchumi, vyote vya nchini na kutoka nje vinaelekezwa katika maendeleo muhimu ya taifa.

Wakati ujao, MKUKUTA unatarajia kwamba asilimia 6 - 8 ya ukuaji kwa jumla kitahitajika kupunguza umasikini. Makisio ya 2007 hadi 2009 yapo katika mpango huu. Tazama jedwali 1 hapo chini. Makisio ya chini ya ukuaji (asilimia 5.9) mwaka wa 2006 yalikuwa kwa sababu ya ukame, ambao uliathiri vibaya kilimo, pia usambazaji wa umeme kwa matumizi ya biashara ya nyumbani.

**Jedwali 1: Makisio ya kukua kwa Pato la Taifa 2006-2009**


| Mwaka | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 |
|---|---|---|---|---|
| **% Ukuaji** | 5.9 | 7.3 | 7.7 | 7.9 |

*Chanzo: Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa Mipango\Bajeti ya 20006/07-2008\09*

## B. Malengo sita yanayoendana na kundi I

Kundi I lina malengo sita yanayoendana. Malengo haya ni:

**Lengo 1**
**Usimamizi mzuri wa uchumi**



**Lengo 2**
**Ukuaji wa uchumi endelevu na mpana**



**Lengo 3**
**Hifadhi ya chakula**



**Lengo 4 na 5**
**Kupunguza umaskini wa kipato vijijini na mijini**



**Lengo 6**
**Nishati ya kuaminika na ya gharama nafuu**




Revenue
2005 2006 2007 2008 2009 2010

## Lengo 1: Usimamizi mzuri wa uchumi

Serikali ya Tanzania inahitaji kusimamia vizuri uchumi wa taifa, ili kuwe na hali nzuri ya wawekezaji, na biashara nyingi na fursa za kazi kwa Watanzania. Misaada kutoka nchi za kigeni (na fedha za kigeni) pia inafaa kutunzwa vizuri na kusimamiwa kwa karibu ili kuongeza fedha kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania.

Kwa jumla, makadirio ya 2005 yanaonyesha uwepo wa hali nzuri ya uchumi, licha ya matumizi makubwa ya fedha za serikali yaliyosababishwa na ukame, kupanda kwa bei ya mafuta, na kuongezeka kwa gharama kutokana na kuahirishwa kwa Uchaguzi Mkuu.

Viashiria vinne muhimu vya kutathmini usimamizi wa uchumi wa Tanzania vimeelezwa hapa chini. Viashiria hivi ni: Mfumuko wa bei, mapato ya serikali, upungufu wa fedha za serikali na mapato yatokanayo na biashara za nje.

### Mfumuko wa bei

MKUKUTA unalenga mfumuko wa bei uwe asilimia 4. Mwaka wa 2005, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.3 lakini kuendelea kwa ukame na kupanda kwa bei ya mafuta kulisababisha mfumuko wa bei kuongezeka mpaka asilimia 6.5 mwezi wa Machi 2006. Hata hivyo, mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua kwa asilimia 4 ifikapo Juni 2007. Kupungua huko kutategemea hali nzuri ya hewa na kuwepo kwa chakula.

### Mapato ya serikali

Mapato yanayokusanywa na serikali ya Tanzania - ambayo ni kodi, ushuru na malipo kwa huduma zinazotolewa na serikali - yaliongezeka kutoka 12.2% ya pato la taifa mwaka wa 2000/2001 mpaka asilimia 13.1 mwaka wa 20004/2005. Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2005/2006 ni asilimia 14.2. Jumla ya mapato yote yaliyokusanywa yameongezeka. Hata hivyo, mapato makubwa zaidi ya ndani yanahitajika ili kupata fedha za maendeleo ya Tanzania kwa miaka ijayo. Mwaka huu na ujao, mapato ya serikali yanaweza kushuka kwa sababu ya upungufu wa biashara kutokana na upungufu wa umeme.



**Mfumuko wa bei ni nini?**

Kiasi cha mfumuko wa bei kwa mwaka mmoja ni jumla ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma kwa mwaka huo. Nchini Tanzania, kuwepo kwa chakula ndiyo jambo muhimu linaloathiri bei za bidhaa na, kwa hiyo, mfumuko wa bei.

Ni muhimu serikali kuchukua hatua kuzuia mfumuko wa bei kwa sababu kupanda kwa bei za bidhaa kunamaanisha jamii zitashindwakupata bidhaa na huduma zinazohitajika.

**Upungufu wa pato la serikali**

Upungufu katika pato la serikali unatarajiwa kushuka kutoka asiliimia 6.6 mwaka 2005/2006 mpaka asiliimia 5 mwaka wa 2006/2007. Lakini kushuka huku kutategemea kuongezeka kwa mapato na matumizi mazuri ya fedha za serikali, na athari zitokanazo na matatizo ya nishati na bei ya mafuta. Kuajiri walimu wengi na wafanyakazi wa afya kutahitaji matumizi makubwa ya fedha. Hivyo, matumizi ya fedha za serikali yatahitaji kutazamwa vizuri na kwa umakini.

**Biashara za nje**

Mapato yatokanayo na biashara za nje yalipanda mwaka 2005. Mauzo ya nje ya bidhaa za kilimo cha asili yaliongezeka kwa karibu asilimia 20 mwaka 2004, na mauzo ya nje ya dhahabu yaliongezeka kufikia milioni US$ 655.5 mwaka 2005. Pia mauzo ya huduma nchi za nje yaliongezeka, sababu kuu ikiwa ni kuongezeka kwa mapato yatokanayo na usafiri na huduma zinazohusiana na utalii. Manunuzi ya bidhaa za nje yaliongezeka wakati huo huo, hasa manunuzi ya mafuta na vifaa.

**Nakisi katika bajeti ni nini?**

Nakisi katika bajeti ni mwanya au tofauti kati ya kiasi cha mapato serikali huchukua na kiasi cha fedha ambacho serikali hutumia kila mwaka. Upungufu huo unaonyesha kiasi cha mikopo serikali inahitaji kuomba ili kufikia matumizi yake.



## Lengo 2: Ukuaji wa uchumi endelevu na mpana

Ili kuendeleza ukuaji wa uchumi, serikali imefanya uwekezaji katika miundombinu kuwa jambo la muhimu. Kiashiria kimoja cha kupanuka kwa miundombinu wa Tanzania – uwezekano wa watu wa vijijini kupata mahitaji yao misimu yote – kitakuwepo katika Bajeti ya Ukaguzi wa Jamii 2007. Hadi hapo MKUKUTA utapima ukuaji wa miundombinu kulingana na hali ya barabara kuu na barabara za mikao. Viashiria vingine viwili vya lengo la pili ni uwekezaji kutoka nje na kiasi cha riba.

**Barabara**

Asilimia ya barabara kuu na barabara za mikoa zilizo katika hali nzuri na ya kuridhisha ilipanda kufikia asiliimia 84 mwaka 2005, kutoka asiliimia 78 katika mwaka 2004. Kutunza barabara hizi ni jukumu la Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Hata hivyo, barabara za vijijini

ambazo ni jukumu la serikali za mitaa, zipo katika hali mbaya kwa jumla. MKUKUTA unatambua kwamba kuwekeza katika reli pia kunaweza kuwa muhimu katika kuboresha usafiri Tanzania.

### Uwekezaji kutoka nje

Uwekezaji kutoka nje ya Tanzania uliongezeka kwa asiliimia 7 mwaka 2005, lakini hili lilikuwa ongezeko dogo kulinganisha na miaka iliyopita. Sababu kubwa ikiwa kupungua kwa uwekezaji katika sekta ya madini. Mpaka sasa, wawekezaji wengi kutoka nchi za nje wamekuwa katika sekta ya madini na utalii, wakati ambapo uwekezaji katika sekta ya kilimo umekuwa mdogo. Uwekezaji mwingi kutoka nje unahitajika katika kilimo ili kuboresha tija na mauzo.

### Kiasi cha riba

Kiasi cha riba kwa mikopo Tanzania bado kipo juu. Mwezi Desemba mwaka 2005, riba iliyotozwa na benki za biashara kwa mikopo ilikuwa asiliimia 11 juu zaidi kuliko riba ambayo benki hulipa kwa kuweka fedha. Hizi riba za juu za kukopa huzuia uwekezaji, hususan kwa biashara za mitaji midogo - na ya kati. Hadi sasa mikopo mingi inatumika kutafuta soko la kilimo au imeshikiliwa na Watanzania walio katika ajira rasmi. Mikopo zaidi inahitaji kuelekezwa kwenye uwekezaji wa ndani ili uzalishaji usaidie biashara kubwa na chache zenye uwezo na kupata mikopo kama mtaji.

## Lengo 3: Hifadhi ya chakula

Lengo muhimu la MKUKUTA ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote wana chakula cha kutosha, kwa kiasi na ubora unaotakiwa. Ukosefu wa chakula ni dalili ya umaskini mpevu,na kaya zilizo na upungufu wa chakula zipo katika hatari ya kukosa afya njema.

Makisio ya chakula yaliyofanywa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Masoko yameonyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka katika miaka michache iliyopita, na uzalishaji kwa 2005/2006 unaonyesha kutosheleza kwa nchi nzima kwa jumla.

Hata hivyo, kuwepo kwa chakula kuna tofautiana sana kutoka wilaya hadi wilaya, na wilaya nyingi zina ukosefu wa chakula. Mwezi Agosti 2005, wilaya 34 (au asilimia 29 ya wilaya zote za Tanzania) ziliripoti upungufu wa chakula. Kufikia Januari 2006, idadi hii iliongezeka mpaka wilaya 77 (asilimia 65 ya wilaya zote) kwa sababu ya ukame wa muda mrefu.

Kuboresha hifadhi ya chakula, mfumo mzuri wa usafirishaji na usambazaji unahitajika kusafirisha chakula haraka kutoka wilaya zenye chakula cha ziada kwenda wilaya zenye upungufu. Usambazaji wa chakula cha msaada unapaswa kulenga kaya zisizokuwa na uwezo wa kupata chakula.

## Lengo 4 na 5: Kupunguza umaskini wa kipato vijijini na mijini

Ili kupunguza umaskini Tanzania, ni muhimu uzalishaji katika kilimo unaongezeka na kudumishwa. Tunahitaji kuwekeza zaidi katika kulima na kusindika mazao.

### Tija ni nini?

Tija hulinganisha uhusiano kati ya vitu vinavyohitajika ili kutoa mazao, kwa mfano, saa zinazohitajika kwa kazi ya kutoa tani moja ya mahindi ni kipimo cha ufanisi katika uzalishaji.

Kwa kuboresha tija, bidhaa nyingi na huduma zinaweza kuzalishwa kwa muda mfupi na gharama nafuu. Ili haya yafanyike, MKUKUTA utahimiza uwekezaji mahususi, kama vile katika elimu ya kuboresha maarifa na stadi kwa wafanyakazi wa Tanzania, na uwekezaji kuongeza kuwepo kwa vifaa bora, na kuongeza matumizi ya mbinu mpya na teknolojia katika kilimo.



### Ukulima wa mkataba

Kumekuwa na mvuto wa kuendeleza mifumo unganishi ya uzalishaji, upanuzi na masoko katika kilimo. Mipango ya wakulima waliounganishwa na makampuni au mashamba makubwa ni mifano ya mifumo hii. Mfano wa mpango wa aina hii wa muda mrefu Tanzania ni wa kiwanda cha sukari. Katika mpango huu, wakulima wadogo walizalisha zaidi ya nusu ya sukari yote Tanzania mwaka 2004/2005, au tani milioni 1.3 za miwa (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tafiti za Kiuchumi). Mazao kama vile chai, mkonge, kahawa na pareto pia yanaendelezwa kwa mipango kama hii.

**Ukulima wa mkataba ni nini?**

Wakulima wadogo Tanzania wanapatwa na matatizo makubwa katika uzalishaji na uuzaji wa mazao yao. Wengi hawawezi kununua vifaa au mashine za uzalishaji, na hawana uwezo wa kushiriki katika maelewano ya bei ya haki kwa mazao wanayouza.

Ukulima wa mkataba, kama vile mpango wa wakulima waliounganishwa na makampuni au mashamba makubwa, ni njia moja ya kuboresha uwezo na mapato ya wakulima. Katika mifumo hii, mashirika makubwa ya kilimo au biashara huwapatia wakulima wadogo mikopo, rasilimali na ushauri wa kiufundi kuboresha uzalishaji. Makampuni hayo kisha hununua mazao ya wakulima wakishavuna.

**Viashiria vingine vya maendeleo ya vijijini**

Sensa ya Kilimo Takwimu kuhusu wakulima wadogo Tanzania (NBS, 2005). Sensa nyingine imepangwa kufanyika 2008. Utafiti uliofanywa 2002/03, ulionyesha kwamba asilimia 3 peke yake ya jumla ya ardhi ya mkulima mdogo inayomwagiliwa. Asilimia 3 ya wakulima wadogo walichukua mkopo kuwekeza katika kilimo. Ili kupata mapato ya ziada, wengi wa wakulima wadogo (asilimia 58) walifanya kazi zingine nje ya mashamba yao.

## Lengo 6: Nishati ya kuaminika na ya gharama nafuu


Nishati ya kuaminika na ya gharama nafuu ni muhimu kwa uchumi, kwa biashara na pia nyumbani. Hata hivyo, upatikanaji wa umeme upo chini – asilimia 10 mijini na asilimia 1 vijijini. Uwezo wa kuzalisha umeme pia uko chini. Mwaka huu ukame ulipunguza ugavi wa umeme utokanao na maji, ambao ni chanzo kikuu cha umeme nchini. Bei ya mafuta pia ilikuwa juu. Matokeo yake, matumiza ya fedha za serikali yalikuwa juu na mapato liyotarajiwa kutokana na kodi yalishuka.

Suala la nishati linastahili kuangaliwa kwa mtazamo mpya na juhudi zaidi zinahitajika ili kutafuta vyanzo vingine vya nishati. Mipango inaendelea kuongeza uwezo wa Tanzania wa kuzalisha umeme, kutafuta vyanzo vingine vya kuzalisha umeme, na kupanua gridi ya taifa. Mwaka 2006 nchi iliweza kutoa kiasi cha 852 Megawatti (MW) za umeme kutokana na nishati ya mafuta na maji. Umeme kiasi cha 13MW hununuliwa kutoka nje – 8MW kutoka Uganda kwenda Bukoba, makao makuu ya mkoa wa Kagera, na 5MW kutoka Zambia huenda Sumbawanga, makao makuu ya mkoa wa Rukwa.

Kutafuta vyanzo vingine vya nishati pia ni muhimu kwa kulinda mazingira ya Tanzania hususan vijijini. Kwa hivyo, kiashiria cha kupima kupungua kwa utegemezi wa kuni na mkaa majumbani kitakuwa katika ripoti zijazo za MKUKUTA.

## KUNDI II: Kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii

Kuboresha huduma za jamii – elimu, afya, maji na usafi – ni kitovu cha kuboresha hali ya maisha na ustawi wa Watanzania wote, kwani ndiyo wajibu wa serikali za mitaa kama watoaji wa huduma za umma katika ngazi ya mtaa.



Maendeleo katika sehemu hii ya mkakati yanapimwa kulingana na malengo 5 yanayobeba kundi 2. Malengo haya ni:

**Lengo 1**
Elimu



**Lengo 2**
Afya



**Lengo 3**
Maji safi na salama, usafi unaofaa, makazi mazuri na uhifadhi wa mazingira



**Lengo 4**
Kulinda makundi maalum na wasiojiweza



**Lengo 5**
Huduma za jamii kwa wote




## Lengo 1: Elimu

Watu wenye elimu ni muhimu kwa maendeleo ya Tanzania, na haki ya kupata elimu inatambulika kisheria katika katiba ya Tanzania.

Jedwali la 3 linaonyesha viashiria vya elimu pamoja na takwimu za hivi karibuni. Kwa ujumla takwimu zinaonyesha mwelekeo mzuri. Ingawaje, tofauti kubwa ya mafanikio ya elimu ni wazi katika maeneo mbali mbali nchini.

### Elimu ya watu wazima

Elimu ya watoto imepewa kipaumbele nchini, hivyo kumekuwa na rasilimali kidogo kwa miradi ya elimu ya watu wazima. Kwa sababu hiyo kujua kusoma na kuandika hakutarajiwi kufikia lengo la MKUKUTA la asilimia 80 ifikapo mwaka 2010. Hata hivyo, miradi ya elimu ya watu wazima haitumii rasilimali nyingi, na faida zake ziko wazi. Kwa mfano, kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kunahusishwa na kuelimika zaidi kwa wanawake.

### Kujiunga katika shule za awali, msingi na sekondari

Kiwango cha kujiunga na shule za awali, msingi na sekondari kimeongezeka zaidi. Asilimia ya wanafunzi wa darasa la VII wanaokwenda sekondari pia imeongezeka.

## Jedwali 2: Viasharia vya elimu vya MKUKUTA

| KISAHIRIA | MSINGI WA KWANZIA UPIMAJI | | MWENENDO | | | | | | MALENGO MKUKUTA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Makadirio | Mwaka | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2010 |
| Kiwango cha watu wanaojua kusoma na kuandika % - Jumla | 71% | 2000/1 | | 69 | | | | Haihusiki | 80% |
| - Wanaume | 64% | 2000/1 | | 62 | | | | Haihusiki | 80% |
| - Wanawake | 80% | 2000/1 | | 78 | | | | Haihusiki | 80% |
| Kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa shule za awali | 24.6 | 2004 | | | | 24.6 | 25.7 | 28.5 | |
| Kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa shule za msingi | 59% | 2000 | 66.5 | 80.7 | 88.5 | 90.5 | 94.8 | 96.1 | 99% |
| Asilimia ya wanafunzi wanaomaliza darasa la 7 | 70% | 2000 | 62.5 | 68.1 | 67.4 | 72.2 | 68.7 | Haihusiki | 90% |
| Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la 7 | 22% | 2000 | 28.6 | 27.1 | 40.1 | 48.7 | 61.8 | Haihusiki | 60% |
| Uwiano wa wanafunzi na walimu | 46:1 | 2000 | | 53:1 | 57:1 | 58:1 | 56:1 | 52:1 | 45:1 |
| Asilimia ya walimu wenye viwango vinavyokubalika | | | 50 | | | 58 | | 69.2 | |
| Kiwango cha kumaliza darasa la 7 na kuingia kidato cha 1 | 21% | 2002 | 22.4% | 21.7% | 30% | 36.1% | 48.7% | Haihusiki | 50% |
| Kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa sekondari | 6% | 2002 | | 5.9 | 6.3 | 8.4 | 10.3 | 13.4 | 50% |
| Asilimia ya wanafunzi waliofaulu kidato cha 4 | 25.8 | 2000 | 28.3 | 36.2 | 38.1 | 37.8 | 33.6 | Haihusiki | 70% |
| Kiwango cha uandikishaji wanafunzi kuingia elimu ya juu | 22,065 | 2000/1 | 2001/2 24,302 | 2002/3 30,083 | 2003/4 39,318 | 2004/5 48,236 | Haihusiki | Haihusiki | |

Mkazo wa rangi unaashiria maendeleo

### Walimu

Kwa elimu ya msingi na ya sekondari, kuna upungufu mkubwa wa walimu, hususan walimu waliohitimu kwa viwango vinavyotakiwa. Ingawa uwiano wa wanafunzi kwa walimu katika shule za msingi unashuka, lakini bado uko juu, ukilinganishwa na lengo la MKUKUTA la mwalimu mmoja kwa kila wanafunzi 45.

### Vitabu vya kiada

Kuongeza vitabu vya kiada ni muhimu katika kuboresha hali ya elimu. MKUKUTA unakusudia kukusanya takwimu bora zaidi kuhusu upatikanaji wa vitabu. Mamlaka za wilaya zinaripoti jumla ya vitabu vya kiada lakini takwimu hizi hazionyesha kama vitabu hivi vimegawanywa ipasavyo kwa wanafunzi.

### Mitihani ya shule

Kiwango cha wanafunzi wanaofaulu mtihani wa mwisho wa shule ya msingi kimeongezeka katika miaka michache iliyopita. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) bila shaka umeleta maendeleo katika vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Uzito wa masomo umebadilika, somo la Kiswahili limepewa uzito zaidi katika mitihani, na wanafunzi wengi hufaulu vizuri somo hili kuliko Kingereza na hisabati. Hata hivyo, ni muhimu kuwe na udhibiti wa ubora katika mitihani ili kuhakikisha kwamba maswali hayawi rahisi.

Kwa upande mwingine kiwango cha kufaulu kwa shule za sekondari katika mitihani ya kidato cha 4 kilishuka. Asilimia ya wanafunzi waliopata daraja la kwanza hadi la tatu ilikuwa asilimia 33.6 mwaka wa 2005, ikilinganishwa na asilimia 38 ya miaka miwili iliyopita.

### Kujiunga na elimu ya juu

Idadi ya wanafunzi wanaojiunga elimu ya juu imeongezeka kufikia wanafunzi 48,236 mwaka wa 2004/2005. Asilimia ya wanawake waliojiunga pia iliongezeka katika miaka mitano iliyopita kutoka asilimia 23.9 hadi asilimia 32.7. Hata hivyo taarifa zaidi zinahitajika. Kwa mfano, tukijua ni wanafunzi wangapi wanahitimu kila mwaka kwa kila somo tutaona kama kweli upungufu katika stadi mbalimbali unashughulikiwa, kama vile katika sekta ya afya.

Serikali inapaswa kutoa fedha zaidi kwa ajili ya elimu ya sekondari na ya juu. Zaidi ya hayo, njia zingine za kupata fedha kwa ajili ya elimu, kama vile mikopo, inapaswa kutafutwa kwa ajili ya elimu na mafunzo yenye manufaa binafsi.

## Lengo 2: Afya

Lengo la MKUKUTA katika afya ni kuweka uzito kwa makundi yenye mahitaji makubwa zaidi kiafya wakiwemo, watoto wachanga na wa umri mdogo, na wasichana na wanawake walio katika umri wa kuzaa. Lengo hili maalum la afya ni sehemu kuu ya lengo pana la MKUKUTA linalohakikisha kwamba huduma za jamii zinapatikana kwa kila mwananchi. Jedwali la 4 linaonyesha viashiria vya MKUKUTA vya afya pamoja na takwimu zake za hivi karibuni.

### Afya ya watoto wachanga na watoto wa umri mdogo

Sensa ya Watu ya mwaka 2002 (NBS 2003) na Utafiti wa Demografia na Afya wa Tanzania 2004/05 (TDHS) (NBS 2005) unaonyesha kwamba vifo vya watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka tano vimepungua. Taarifa zinazotoka TDHS zinaashiria kuwa sababu kuu ya kupungua huko inaweza kuwa ni jitihada za kutoa huduma za kinga dhidi ya malaria (watoto na wanawake wajawazito kutumia chandarua zilizowekwa dawa ya malaria) pamoja na matibabu ya ugonjwa huu.

Hata hivyo kuna tofauti kubwa kati ya idadi ya vifo vya watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano katika wilaya na mikoa mbali mbali. Katika wilaya 15, (Idadi kubwa ya mikoa hii ipo upande wa kusini mashariki mwa nchi), kiasi cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano ni vifo 200 au zaidi kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa. Katika wilaya za Rungwe, Dodoma vijijini pamoja na Mtwara vijijini mtoto mmoja kati ya wanne hufa kabla hajafikia umri wa miaka mitano. Ikilinganishwa na wilaya zilizopo kaskazini mashariki, idadi ya vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano ni watoto 50 kwa kila watoto 1000. Idadi hii imepungua mara nne ya ile ya kusini mashariki. Hatua zaidi zinapaswa kuchukuliwa haraka ili kuokoa maisha ya watoto.

Utapiamlo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano umeongezeka. Watoto wanne kati ya 10 wamedumaa na hii ni dalili ya ukosefu wa lishe kwa muda mrefu.

Cha muhimu ni kwamba kipindi ambapo watoto na wazazi hufika katika vituo vya afya mara kwa mara ndiyo wakati huo huo watoto wachanga huathirika na utapiamlo. Na kufuatia hayo, utafiti uliofanywa hivi karibuni unasisitiza kwamba huduma za afya zinapaswa kutilia maanani uchunguzi na kinga ya utapiamlo kwa watoto.

Chanjo inastahili kuenea pote na kiwango kilichofikiwa Tanzania ni cha juu.

**Utapiamlo au ukosefu wa chakula cha kutosha ni nini? Kudumaa ni nini?**

Utapiamlo au ukosefu wa lishe bora hutokea wakati watu hawapati chakula cha kutosha chenye lishe itakayoweza kuhimili kukua kwa kawaida – yaani, chakula cha kutosha chenye protini, nguvu, vitamini na madini.

Chakula ndiyo kichochezi cha miili yetu kukua na ndiyo chanzo cha kuwepo kwa afya. Sote tunahitaji chakula kizuri chenye virutubisho vya kutosha, hasa watoto. Mtoto mchanga akikosa chakula chenye virutubisho vya kutosha, mwili wake hudumaa. Kudumaa kunaonekana pale ambapo mtoto ni mfupi akilinganishwa na watoto wa umri wake. Kudumaa huanzia miezi mitatu, na kunaweza kuendelea hadi mtoto anapofikia umri wa miaka miwili au mitatu. Hata hivyo, ni vigumu kwa watoto kupona au kupata nafuu wakidumaa wakiwa wachanga sana, na hali hii inaweza kuwa na athari ya muda mrefu kwa watoto, kwa mfano uwezo wa akili na kufikiri.



## Jedwali 3: Viasharia vya afya vya MKUKUTA

| KISAHIRIA | MSINGI WA KWANZIA UPIMAJI | | MWENENDO | | | | | | MALENGO MKUKUTA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Makadirio | Mwaka | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2010 |
| Idadi ya vifo vya watoto wachanga katika kila watoto 1000 wanaozaliwa | | | | | | | | | |
| - TDHS* | 99 | 1999 | | | | 68 | | Haihusiki | 50 |
| - Sensa | | | | 95 | | | | | |
| Idadi ya vifo vya watoto walio-chini ya miaka 5 katika kila watoto 1000 wanaozaliwa | | | | | | | | | |
| - TDHS* | 147 | 1999 | | | | 112 | | Haihusiki | 79 |
| - Sensa | | | | 162 | | | | | |
| Asilimia ya utoaji chanjo dhidi ya Surua na DPT | | | | | | | | | |
| Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 78% | | | | | 80 | 85 | Haihusiki | 85% |
| - TDHS* | 81% | 1999 | | | | 86 | | | |
| Kiwango cha watoto walio - chini ya miaka 5 wenye kimo pungufu | 44% | 1999 | | | | 38 | | Haihusiki | 20% |
| Kiwango cha wanaojifungua wanaohudumiwa na watumishi wenye ujuzi | 36% | 1999 | | | | 46 | | Haihusiki | 80% |
| Asilimia ya watu wenye VVU wanaopata dwa za kupunguza makali | | | | | | Kuanza kwa programu | | Kufikia Agosti, 48% ya lengo | 100,000 Kufikia Dec '06 |
| Asilimia ya kuenea kwa VVU miongoni mwa kundi la wenye miaka 15 -24 | | | | | | | | | |
| - Uchunguzi wa VVU/UKIMWI Tanzania | | | | | 3.5 | | | Haihusiki | 5 |
| Wachangiaji damu | | | 9.1 | 7.4 | 6.7 | 7.4 | | | |
| Asilimia ya kuponyesha kwa matibabu ya Kifua Kikuu | 81% | 2001 | | | 80.9 | | | Haihusiki | |

* TDHS = Uchunguzi kuhusu ya hali ya jamii na afya Tanzania

Mkazo wa rangi unaashiria maendeleo

### Afya ya Uzazi

Kiwango cha vizazi vilivyotokea chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya kiliongezeka hadi asilimia 46 mwaka 2004/2005, lakini kiwango hicho bado kiko chini ikilinganishwa na lengo la MKUKUTA la asilimia 80. Kuna uwezekano mkubwa kwa wanawake walio mijini na wasio maskini kujifungua katika mikono ya mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi. Kuwepo kwa huduma za kiafya wakati wanawake wanajifungua ni jambo linalohitaji kupewa kipaumbele ili kupunguza idadi ya ulemavu na vifo vitokanavyo na uzazi Tanzania.

**UKIMWI**

Ukitambua umuhimu wa kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya Ukimwi, MKUKUTA umetoa taarifa kuhusu hali ya maambukizi kwa watu wenye umri kati ya miaka 15-24. Kiashiria hiki kimetumiwa kukadiria kiwango cha watu wapya walioambukizwa. Taarifa za Utafiti wa kwanza wa maambukizo ya Virusi Vya Ukimwi (VVU)/UKIMWI Tanzania mwaka 2003/2004 zilionyesha asilimia 3.5 kwa kundi hili. Utafiti mwingine umepangwa kufanyika 2007/2008.

Viwango wa maambukizi ya UKIMWI pia hukadiriwa kwa njia ya kupima damu kutoka kwa watoaji damu. Makadirio kwa njia hii yapo juu: asilimia 7.4 mwaka 2004. Hii inaweza kuwa kwa sababu watoaji wengi wa damu hutoka mijini, ambapo maambukizo ya ukimwi yapo juu ikilinganishwa na idadi ya walioambukuzwa vijijini.

Jitihada za kuzuia kuenea kwa janga la UKIMWI zimevuta fedha nyingi za kigeni, katika suala la matibabu. Hata hivyo, kuna wasiwasi kwamba fedha hizi zipo kwa muda mfupi tu. Serikali ilikuwa imelenga watu 100,000 walioathirika na UKIMWI kupata dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARV) ifikiapo mwisho wa mwaka 2006. Hadi Agosti mwaka 2006, jumla ya watu 48,000 tu walikuwa wanapata matibabu.

## Lengo 3: Maji safi na salama, usafi unaofaa, makazi mazuri na ulinzi wa mazingira.

**Maji safi na salama**

Upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mambo muhimu kwa jamii, hasa katika maeneo ya vijijini. Takwimu zilizopatikana kutoka sensa ya mwaka 2002 na TDHS mwaka 2004/2005 zinaonyesha kwamba nusu ya watu wanaoishi vijijini na robo ya watu mijini na jijini hawapati maji safi. Hiki ni kipaumbele kinachohitaji rasilimali nyingi zaidi. Ifikiapo mwaka 2010, MKUKUTA unalenga asilimia 90 ya wakazi wa mjini na asilimia 65 ya watu wa vijijini kupata maji safi na salama yatakayopatikana karibu na makazi yao, yasiyozidi mwendo wa dakika 30 kuyateka na kurudi nyumbani mwao.

**Usafi unaofaa**

MKUKUTA unalenga kuhakikisha kwamba asilimia 95 ya Watanzania wanakuwa na mambo ya msingi katika usafi ifikiapo mwaka 2010. Takwimu za hivi karibuni zilionyesha kwamba karibu asilimia 90 ya jamii tayari wana mambo ya msingi katika usafi, lakini takwimu hizi zinajumuisha jamii zenye aina yoyote ya vyoo na hazizingatii kama vyoo hivi vinatumiwa na kila mmoja katika jamii hiyo.

Lengo lingine la MKUKUTA ni kujenga vyoo vya kutosha katika kila shule ifikapo mwaka 2010. Kulingana na viwango vilivyowekwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kila shule

lazima iwe na choo kimoja kwa wasichana 20, na choo kimoja kwa wavulana 25. Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kwamba asilimia 66 za shule za msingi hazijafikia kiwango hiki. Hadi sasa, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi unasisitiza ujenzi wa madarasa, lakini vyoo ni vya umuhimu pia, hasa kwa wasichana.

**Jedwali 4: Viasharia vya maji na usafi vya MKUKUTA**

| KISAHIRIA | MSINGI WA KWANZIA UPIMAJI: Makadirio | MSINGI WA KWANZIA UPIMAJI: Mwaka | MWENENDO: 2001 | MWENENDO: 2002 | MWENENDO: 2003 | MWENENDO: 2004 | MWENENDO: 2005 | MWENENDO: 2006 | MALENGO MKUKUTA 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watu wenye uwezo wa kupata maji safi na salama (katika muda wa dakika 30 kwenda, kuchota maji na kurudi) | Mijini 73%<br>Vijijini 53%<br>Mita 200 kutoka chanzo cha maji | 2000/1 | | Mijini 85%<br>Vijijini 42%<br>Takwimu za sensa | Mijini 73%<br>Vijijini 53%<br>Takwimu za ki-utawala | | | Haihusiki | Mijini 90%<br>Vijijini 65% |
| Asilimia ya kaya zenye huduma za msingi za usafi | 91% | 2002 | | 91 | | | | Haihusiki | 95% |
| Aslimia ya shule zenye vyoo (kwa mujibu wa muongozo wa Wizara ya Elimu na ustawi wa Jamii) | | | 35.7 | 36.2 | 32.8 | 36.7 | | Haihusiki | 100%* |
| Idadi ya kesi za ugonjwa wa kipindupindu zilizoripotiwa (kiwango kwa kila watu 100,000) | | | 6.9 | 28.5 | 35 | 20.9 | | Haihusiki | Kupunguza milipuko kwa nusu kufikia 2010 |

* Uwiano wa 1:20 wasichana; 1:25 wavulana

Mkazo wa rangi unaashiria maendeleo

## Kuhifadhi mazingira

Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kuwa Tanzania ina rasilimali kubwa zisizotumiwa, na rasilimali hizi zinahitaji kusimamiwa kwa uangalifu ili kukidhi mahitaji ya watu waliopo na wa kizazi kijacho cha Watanzania (Benki Ya Dunia, 2005). Ni muhimu kutochafua au kuharibu vyanzo vya maji, ardhi na udongo, misitu na rasilimali zingine. Utunzaji wa mazingira utasaidisa kutunza makazi na kupunguza athari zitokanazo na majanga ya asili kama vile ukame na mafuriko.

Hivyo basi, MKUKUTA unao kiashiria – usimamizi wa rasilimali kupitia jamii – ambacho kinahusisha ukuaji wa uchumi na utunzaji wa mazingira. Kiashiria hiki kitashughulikia maswala mengi ya mazingira, yakiwemo ya maji, misitu, wanyama pori na sehemu za uvuvi, pamoja na maendeleo ya utalii.

Hivi sasa, taarifa zilizopo ni chache isipokuwa zile zinazohusu misitu ya Tanzania. Makisio ya eneo la misitu na eneo lenye miti nchini ni karibu hekta milioni 40, ambapo, hekta milioni 15 ni ardhi ilivyohifadhiwa kwa matumizi maalum ambayo yanaweza kufaidika kutokana na usimamizi chini ya Sheria ya Misitu. Hata hivyo, mwaka 2001 karibu hekta 600,000 zilikuwa chini ya usimamizi wa serikali ya mitaa, na asilimia 1 ya misitu kwa jumla ipo chini ya usimamizi wa jamii au usimamizi wa pamoja kati ya jamii na vikundi mbalimbali. Utaratibu na kanuni za kutekeleza sheria hii unatayarishwa. Serikali kuu inahitaji kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa ardhi na wanyama pori pamoja na kupanga na kukusanya ushuru.

## Lengo 4: Kulinda makundi maalum na wasiojiweza

Serikali inafahamu kwamba Watanzania wote wanapaswa kulindwa dhidi ya umaskini uliokithiri, ubaguzi na kutengwa, na MKUKUTA umeweka kwa mara ya kwanza lengo la kitaifa la ulinzi wa jamii.

Serikali itaanza kwa kutilia mkazo kusaidia makundi ya watu wasiojiweza katika jamii zetu - wanawake na watoto (hususan yatima), wazee, walemavu na wagonjwa.

### Watoto kufanyishwa kazi

Ni watoto chini ya umri wa miaka 18 wanapofanyishwa kazi isiyolingana na umri wao, na ambayo inawanyonya, kuhatarisha na kukwaza masomo na kukua kwao. MKUKUTA unajaribu kupunguza kiwango cha watoto wanaofanya kazi kufikia chini ya asilimia 10. Utafiti uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka wa 2002/2003 uligundua kwamba biashara za kilimo, uchimbaji madini, kazi za nyumbani, biashara ya ngono, na sekta isiyo rasmi mijini ndiyo maeneo yanayohusishwa na watoto kufanyishwa kazi.

### Watoto walemavu

Utafiti wa hivi karibuni wa sensa za Tanzania (Lindeboom et.al, 2006) ulionyesha kwamba watoto walemavu hupata elimu ndogo kuliko watoto wasiokuwa walemavu. Ili kutatua tatizo hili MKUKUTA unalenga kuwezesha asilimia 20 ya watoto walemavu kuhudhuria shule ifikapo mwaka wa 2010. Takwimu za hivi karibuni kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zinaonyesha kwamba watoto walemavu 18,291 wanahudhuria shule za msingi. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na watoto walemavu walioko Tanzania.

### Watoto yatima

Takwimu kutoka utafiti wa TDHS mwaka 2004/2005 zinaonyesha kwamba asilimia 8.5 ya watoto wa Tanzania ni yatima, yaani wamepoteza mzazi mmoja ama wote. Takwimu hizi zinakaribiana na takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi mwaka 2006 zilizoonyesha kwamba asilimia 9.4 ya watoto waliohudhuria shule ni yatima. Zikiangaliwa kwa pamoja, takwimu hizi zinaonyesha kwamba yatima hawatakuwa na kiwazo kikubwa kuhudhuria

shule, kama jamii inawaunga mkono. Hata hivyo, utafiti zaidi unahitajika ili kuangalia mahitaji ya yatima, hususan wale waliopoteza wazazi wao kwa ugonjwa wa ukimwi. Kwa mfano, utafiti unaonyesha kwamba watoto waliopoteza mama zao wapo katika hatari kubwa zaidi ya kunyanyaswa. Kuwa yatima katika umri mdogo pia kunawaweka watoto katika hali ngumu zaidi.

**Wazee**

MKUKUTA unalenga kuwapatia wazee matibabu ya bure katika hospitali za umma. Jamii inapaswa kuwatambua wazee ambao hawana uwezo wa kugharamia matibabu yao, ili waweze kufaidika na huduma hii. Takwimu za idadi ya wazee wanaopata matibabu ya bure zitachukuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2007.

Ili kufikia shabaha ya asilimia 100 ya MKUKUTA, sera iliyo wazi na yenye ukamilifu inahitajika. Wadau wote - wazee, familia zao, wafanyakazi wa serikali za mitaa na wafanyakazi wa afya - lazima wajue ni nani anayestahili kupata huduma bure. Pia, mfumo lazima uwepo ili gharama ambazo hospitali na vituo vya afya huingia kwa kutibu wagonjwa wazee ziweze kurejeshwa.

## Lengo 5: Huduma za jamii kwa wote

MKUKUTA inatambua kwamba kila mwananchi anapaswa kupata huduma bora za jamii. Taarifa zinazoweza kutumika kukadiria maendeleo kuhusu lengo hili ni finyu kwa wakati huu, lakini Utafiti wa Bajeti ya Kaya mwaka 2000/2001 (*NBS, 2002*) uliuliza kama Watanzania wanaridhika na huduma za afya. Hata hivyo, utafiti huu haukuelezea kwa nini watu huamua kutotafuta huduma za afya.

Kwa ujumla, karibu theluthi mbili za watu walioshiriki katika utafiti huu wameridhika na upatikanaji wa huduma za afya. Waliohojiwa walieleza kuridhika na huduma zinatolewa na maduka ya dawa, ikifuatiwa na huduma zinazotolewa na madaktari wa meno na madaktari binafsi. Watu hawakuridhika na huduma za hospitali za mikoa na vituo vya afya vya umma. Malalamiko makubwa yalikuwa kuhusu bei za hospitali za mikoa na ukosefu wa madawa katika vituo vya afya vya umma.

Kila binadamu ana haki ya kupata huduma za jamii.



## KUNDI III: Utawala bora na uwajibikaji

Kama ilivyoelezewa katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii, kufanikiwa kwa kundi la kwanza na la pili la MKUKUTA kunategemea utawala bora. Utawala bora ni mazingira ambayo ukuaji wa uchumi, ubora wa hali ya jamii, na upunguzaji wa umasikini kunaweza kufanyika.

Mwaka huu wa 2006 ndiyo wa kwanza ambao juhudi za kupata utawala bora nchini kote zinafuatiliwa. Hii inaonyesha kupiga hatua kubwa mbele. Matokeo ya awali yanaonyesha picha ya jumla ya mafanikio ya kuridhisha, lakini juhudi zaidi zinatakiwa ili hali hii iendelee kuwa bora.

Moja ya changamoto kubwa ni ukosefu wa taarifa kutoka serikali za mitaani. Ingawa viashiria vimekubaliwa, bado taarifa hazitiririki vizuri kati ya mfumo wa usimamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PMO-RALG) na mfumo wa usimamizi wa MKUKUTA. Juhudi zaidi zinahitajika ili kuboresha mawasiliano kati ya mifumo hiyo miwili.

Katika maeneo mengi, upatikanaji wa takwimu umekuwa mgumu, lakini taarifa zote zilizopo zimekusanywa na kuchambuliwa kulingana na malengo saba yanayounda kundi III la MKUKUTA.

Kundi III lina malengo 7. Malengo haya ni:

- **Lengo 1** Utawala na utawala wa sheria
- **Lengo 2** Mgawanyo sawa wa rasilimali za umma na kupungua kwa rushwa
- **Lengo 3** Utumishi wa umma wenye ufanisi
- **Lengo 4** Haki za masikini na wenye mahitaji maalum katika mfumo wa sheria
- **Lengo 5** Kupunguza kutengwa kisiasa na kijamii na kuto-vumiliana
- **Lengo 6** Kuboresha usalama, kupunguza uhalifu na kuondoa unyayasaji wa kijinsia na ukatili majumbani
- **Lengo 7** Kudumisha utambulisho wa kiu-tamaduni wa taifa




Is someone you
love pregnant?
Every hour about one girl or woman
in Tanzania dies from pregnancy or

## Lengo 1: Utawala na utawala wa sheria

MKUKUTA unafanya kazi kuhakikisha kwamba taasisi za serikali na mifumo yao ni ya:

- Kidemokrasia
- Shirikishi
- Wakilishi
- Uwajibikaji
- Jumuishi

Viashiria vya lengo vinajumuisha usajili wa vizazi na vifo, uwakilishaji wa wanawake bungeni na kwenye utumishi wa umma, usawa wa jinsia, na uwajibikaji wa viongozi wa serikali za mitaa.

**Usajili wa vizazi**

Cheti cha kuzaliwa ni hati muhimu sana ya kutambulisha uraia. na usajili unahitajika ili watoto wako waruhusiwe katika shule za msingi. Hivyo basi, serikali inafahamu kwamba usajili wa vizazi ni haki ya Watanzania wote. Usajili pia hutoa habari muhimu kuhusu idadi ya watu nchini ili serikali iweze kupanga ipasavyo huduma zake.

Takwimu za hivi karibuni (TDHS, 2004/2005) zinaonyesha kwamba usajili ulikuwa wa chini sana, hasa nje ya Dar es Salaam. Ni asilimia 5.7 tu ya wanaozaliwa ndiyo wamesajiliwa. Usajili pia huwa chini sana vijijini - chini ya asilimia 3 - ikilinganishwa na asilimia 20 mijini. Ingawa usajili ni wa bure wakati wa kuzaliwa na mpaka siku tisini baada ya kuzaliwa, wazazi wachache tu ndiyo husajili watoto wao mapema.

Kwa hiyo, juhudi kubwa zinahitajika kueleza wazazi umuhimu na faida za kusajili watoto wao wote. MKUKUTA pia utajitahidi kupunguza ugumu wa kusajili kwa kuboresha namna ya kuzifikia ofisi za kusajili kwa jamii za vijijini, na kupunguza gharama za usajili wa waliochelewa. Njia moja ni kuunganisha usajili wakati wa kuzaliwa na chanjo kwa mtoto, ili zote zifanywe kwa wakati mmoja.

**Wanawake bungeni na katika utumishi wa umma**

Idadi ya wanawake wanaowakilisha bungeni imeongezeka taratibu tangu baada ya uhuru. Mwaka 2005, karibu theluthi moja ya wabunge wote walikuwa wanawake, ambayo ni uwiano mkubwa sana ikilinganishwa na idadi katika nchi nyingine za Afrika Mashariki. Pia, mawaziri wengi wa kike waliteuliwa baada ya uchaguzi wa mwaka 2005 kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya Tanzania. Kati ya mawaziri 29 waliopo bungeni, sita ni wanawake.

Uwakilishi wa wanawake katika utumishi wa umma umeongozeka, lakini wanawake wengi serikalini wanapatikana katika ngazi za katikati na za chini. Juhudi na mafunzo maalum yanahitajika ili wanawake serikalini waweze kushindania nafasi za juu na kupandishwa vyeo katika hali ya usawa.

### Usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi

Nchini Tanzania asilimia 58 ya wakazi vijijini hutumia ardhi chini ya sheria ya ardhi ya mila; asilimia 16 wamenunua ardhi, na asilimia 26 ya wakazi waliobaki wamekodisha au wana mkataba wa kukodi nyumba au kukodi shamba na kugawana mazao. Asilimia 5 ya wakazi ndiyo wenye hati rasmi ya kumiliki ardhi (Sensa ya Kilimo 2002/2003).

Kupima usawa wa kijinsia katika kumiliki ardhi kunakabiliwa na changamoto kadhaa. Kwanza, umiliki wa ardhi hasa vijijini, mara nyingi huchukuliwa kama haki ya anayetumia ardhi hiyo. Pia, sheria ya ndoa ya Tanzania na sheria za kurithi zinazuia haki ya mke kurithi ardhi baada ya kifo cha mumewe. Sheria hizi zilipaswa kupitiwa na kufanyiwa marekebisho kabla ya kuanza kwa MKUKUTA, lakini mabadiliko yamekuwa madogo.

**Usawa ni nini? Usawa wa kijinsia ni nini?**

Usawa ni hali ya kutopendelea na kuwepo kwa haki. Usawa wa kijinsia ni hali ambayo wajibu na faida zinagawanywa kwa haki na bila upendelevu kwa wanawake na wanaume katika jamii. Kwa mfano, wote wanawake na wanaume wanapaswa kuwa na haki ya kumiliki na kurudhi ardhi, na watoto wa kike na wa kiume wanapaswa kupata elimu shuleni.



### Uwajibikaji wa mamlaka ya serikali za mitaa

Mamlaka za serikali za mitaa zinawajibika kutoa taarifa zinazohusu fedha – ikiwa ni pamoja na bajeti, mapato yanayokusanywa, na matumizi - kwenye mbao za matangazo. Hata hivyo uchunguzi umeonyesha kwamba ni taarifa chache zinazotolewa vijijini. Ubora wa taarifa hizo na muda zinapotolewa haziendani. Juhudi nyingi kutoka TAMISEMI, na asasi za kiraia zinahitajika kuboresha sehemu hii ya uwajibikaji kwa umma.

## Lengo 2: Mgawanyo sawa wa mali ya umma na kupungua kwa rushwa

Maendeleo yamepatikana kufikia lengo hili na juhudi zinaonekana zipo katika mwelekeo unaofaa. Mapato yanayokusanywa na serikali, kuboreshwa kwa manunuzi ya serikali, ukaguzi za hesabu za serikali, na juhudi za kupambana na rushwa ni kati ya viashiria vya kupima maendeleo.

### Ukusanyaji wa mapato

Kiasi cha kodi kinachokusanywa na serikali kinazidi kuongezeka taratibu, lakini viwango vya kodi inaokusanywa ipo chini zaidi ya nchi zilizolingana kiuchumi na Tanzania. Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza misingi ya ukusanyaji kodi na pia kupunguza mianya inayoruhusu kodi iliyokusanywa kupotea, kudanganya kulipa kodi, pamoja na kukwepa kulipa kodi.

Changamoto kubwa iliyopo ni kukadiria mapato yaliyobaki. Katika kutekeleza hili, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inashughulikia suala la kutekeleza viwango vya kimataifa katika uendeshaji wa shughuli za kodi.

## Manunuzi ya serikali

Hatua za msingi za kuboresha mfumo wa manunuzi ya serikali zimechukuliwa katika miaka michache iliyopita. Chini ya Sheria mpya ya Manunuzi ya mwaka 2004, Wizara za Serikali pamoja na serikali za mitaa zina madaraka ya kufanya manunuzi.

Kwa ujumla mabadiliko yamekuwa yakuridisha, lakini utendaji kazi wa bodi za zabuni unapaswa kuboreshwa. Utoaji zabuni ngazi ya serikali za mitaa pia unahitaji kufanyiwa marekebisho ya kueleweka. Pamoja na hayo, uwekaji wa kumbukumbu katika hifadhi za serikali unapaswa kuboreshwa kwani hapakuwepo na maelezo ya matumizi ya fedha za serikali ya shilingi bililoni Tsh3.6 mwaka 2004/5.

## Ukaguzi za hesabu za serikali

Mwaka 2003/2004, asilimia 45 ya hesabu za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali zilikuwa safi, hili ni ongezeko kubwa kutoka asilimia 24 mwaka 1998/1999. Mwelekeo wa serikali za mitaa pia unaonyesha maendeleo. Ukaguzi wa vitabu mwaka 2003/2004 ulionyesha kuwa asilimia 43 ya hesabu za serikali za mitaa zilikuwa safi. Idadi hii imeongezeka kutoka asilimia 9 ya 1998/1999. Hata hivyo, uwezo wa serikali za mitaa kusimamia fedha zake unapaswa kuboreshwa, hususan wakati wanapopata fedha nyingi kutoka serikali kuu na kwa wafadhili.

Taarifa zinazotolewa na TAMISEMI kwa wakati huu ni finyu. Mtiririko wa fedha na utaratibu wa kutoa taarifa wa TAMISEMI unahitaji kunyooshwa, kuimarishwa na kuwekwa wazi. MKUKUTA unatambua umuhimu wa usimamizi makini wa fedha na matumizi ya TAMISEMI kwa sababu zina jukumu la kutoa huduma muhimu kwa umma.

### Ukaguzi wa hesabu ni nini?

Ukaguzi wa hesabu ni uchunguzi rasmi wa utaratibu wa matumizi ya shirika au ya mtu binafsi ili kuhakikisha kwamba maamuzi na matumizi ya fedha yanakubaliana na sheria na taratibu zinazohusika.



**Rushwa**

Mwaka 2006, utafiti wa maoni kuhusu hali ya rushwa ulifanywa (Afrobarometer, 2006). Utafiti huo ulionyesha kuwa:

- Asilimia 66 ya Watanzania wanafikiri kwamba siyo sahihi kwa ofisa wa serikali kupeleka mradi wa maendeleo sehemu ambayo marafiki na wafuasi wake wanaishi;
- Asilimia 69 ya Watanzania wanafikiri kwamba siyo sahihi kwa ofisa wa serikali kuwapa kazi watu wa familia yake au watu wasio na sifa;
- Asilimia 72 wanaona siyo sahihi kwa ofisa wa serikali kudai kitu chochote au malipo zaidi kwa huduma ambazo wanapaswa kutoa ikiwa ni sehemu ya kazi zao za kila siku;
- Washiriki walibanisha kwamba hatua zinapaswa kuchukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kufunguliwa mashtaka au kupewa adhabu.

Watanzania pia waliona kuwa kuna rushwa ya hali ya juu katika sekta ya umma. Watu wanne kati ya watano waliohojiwa walifikiri kuwa kuna rushwa katika jeshi la polisi, wakati asilimia 71 wanafikiri kuwa kuna rushwa katika idara ya mahakama. Hata hivyo, matukio ya rushwa yaliyofikishwa mahakamini katika ngazi ya mikoa mwaka 2005 yalikuwa machache sana.

Marekebisho katika sekta ya kutoa haki yanahitajika kwa haraka. Ili kupambana na rushwa, mambo mawili yanahitaji kushughulikiwa. Ukosefu wa ulinzi kwa watu wanaofichua vitendo vya rushwa ni dosari kubwa katika mfumo wa haki na unahitaji kuangaliwa. Serikali ina mipango ya kutunga sheria itakayoangalia suala hili. Lingine ni kwamba mipango na miundo ya kuwezesha asasi za kiraia kujiunga na mapambano dhidi ya rushwa ni dhaifu.

## Lengo 3: Utumishi wa umma wenye ufanisi

Tangu miaka 1990, hatua muhimu zimechukuliwa kuboresha uwezo wa Serikali kutoa huduma. Hata hivyo, marekebisho katika malipo ya mishahara yamekuwa taratibu sana. Utumishi wa umma unaendelea kupoteza wataalamu wanaohamia kwenye kazi zinazolipa vizuri katika sekta binafsi. Aidha, wafanyakazi wengi wanaofanya katika utumishi wa umma hawafanyi kazi kwa uwezo wao wote kwa sababu ya malipo madogo.

Kwa sasa Tanzania ina tatizo la upungufu mkubwa wa walimu na wafanyikazi wa afya, yakiongezewa pia matarajio makubwa ya mishahara mizuri na hali nzuri za kufanya kaz. Serikali inapaswa kutafuta watoaji wa huduma zingine kwa baadhi ya huduma ambazo hapo awali ilikuwa ikizitoa. Kwa mfano, sehemu nyingine za elimu ya juu zinaweza kugharamiwa kupitia mifumo ya mikopo.

Ili iweze kubakisha wataalamu na kuboresha utoaji wa huduma, serikali ilianzisha tume ya Rais mwaka 2006, na kuzindua awamu ya pili ya marekebisho ya huduma ya umma. Hata hivyo,

kwa mapendekezo yoyote yatakayotolewa inabidi ieleweke kwamba mahitaji katika bajeti ya taifa yanazidi uwezo uliopo, hivyo vipaumbele lazima vizingatiwe.

**Kuridhishwa na huduma za serikali**

Kuridhika kwa wateja ni kiashiria muhimu cha maendeleo katika utoaji wa huduma za umma. Watanzania waliripoti maboresho katika chanjo, elimu, ukusanyaji kodi, ukarabati wa barabara na huduma za wakunga wa jadi. Hata hivyo, utoaji wa huduma za serikali unatofautiana sana na pia ukosefu wa watoa huduma ni tatizo kubwa.

Kwa ujumla, watu hawakuridhika, na wakaripoti tabia za rushwa, pale walipokutana na watoaji wa huduma; kwa mfano, huduma zinazotolewa na polisi, maafisa wa uhamiaji na wahudumu wa afya. Zaidi ya nusu watu waliojibu hawakuridhika na huduma hizi. Watu wengi pia walionyesha kutoridhishwa na huduma katika shule za sekondari ikilinganishwa na shule za msingi.

Ili kuboresha utoaji wa huduma, inapendekezwa kwamba Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na TAMISEMI waandae bajeti na wafanye utafiti mara kwa mara kuhusu kuridhika kwa wateja wanaopata huduma za umma.

## Lengo 4: Haki za masikini na wenye mahitaji maalum katika mfumo wa sharia

Hivi sasa Tanzania, ina mlolongo wa kesi za jinai na za madai za siku zilizopita ambazo hazijasikilizwa, na jela zetu zimejaa kupita kiasi. Mwaka 2005, asilimia 16 ya watu waliowekwa rumande – hawa ni wale ambao hutiwa mbaroni hadi kesi zao zitakaposikilizwa kortini – walikuwa wamekaa jela zaidi ya miaka miwili. MKUKUTA unalenga kupunguza kiwango hiki hadi asilimia 7.5, hii itasaidia kupunguza msongamano uliopo ndani ya magereza. Hata hivyo, utoaji wa haki unastahili kuharakishwa, na wafanyakazi zaidi waliofuzu katika sheria wanahitajika.

Watoto wanaovunja sheria ni changamoto kwa serikali kwa sababu ya ukosefu wa jela zinazowafaa. Maeneo ya mikoa ya kati, magharibi na kaskazini magharibi hayana jela tofauti kwa watoto waliovunja sheria.

Ili kutatua haya matatizo, jela zinapaswa kuongezeka, ama njia zingine kubuniwa za kuzuia uhalifu ama kuadhibu wahalifu kama vile kutoa huduma kwa jamii. Utekelezaji wa mapema wa mpango uliosubiriwa kwa muda mrefu wa mabadiliko ya sekta ya sheria unahitajika ili uharakishe utoaji wa haki Tanzania.

## Lengo 5: Kupunguza kutengwa kisiasa na kijamii na kutovumiliana

Kiashiria cha lengo hili ni idadi ya kesi zilizopo katika majalada kwa uvunjaji wa haki za binadamu. Mwaka 2005, tume ya haki za binadamu na utawala bora ilipokea malalamiko 12,434, kati ya haya iliamua 7,111. Kwa kawaida ni kesi chache sana za haki za binadamu zinazofika mahakamani. Hata hivyo, takwimu hizi zinaonyesha ya kwamba wananchi wanafahamu haki yao ya kushitaki.

Kwa miaka ijayo, elimu kwa umma kuhusu maadili ya haki za binadamu na utawala bora inaweza kusaidia kupunguza kutovumiliana na kutengana katika siasa na jamii.

## Lengo 6: Kuboresha usalama, kupunguza uhalifu na kuondoa unyanyasaji wa kijinsia na ukatili majumbani

MKUKUTA unalenga kupunguza uhalifu na kuboresha usalama kwa kuwapa polisi mafunzo na vitendeakazi, kuwabadilishia wafungwa ahadbu, badala ya kutumikia vifungo vyao jela kwa kufanya kazi za umma. Kama ilivyotajwa hapo awali, jela za Tanzania zimejaa kupita kiasi na zipo katika hali mbaya. Kwa wastani, idadi ya wafungwa walio gerezani ni mara mbili zaidi ya uwezo wa jela hizo.

Takwimu za vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na ukatili wa majumbani bado hazijapatikana. Hata hivyo, mwaka 2004-2005 TDHS ilionyesha kiwango cha kushtua cha majibu kuwa asilimia 42 ya wanaume na asilimia 60 ya wanawake – wanaona kitendo cha mume kumpiga mke wake ni sawa. Utafiti uliofanywa Dar es Salaam na Mbeya mwaka 2006 pia ulionyesha kwamba kiwango kikubwa cha wanawake walishawahi kupigwa ama kudhalilishwa kijinsia na wenzi wao. Ili kutataua tatizo hili, MKUKUTA unalenga kuifahamisha zaidi jamii kuhusu haki za wanawake, pamoja na haki zao za kulindwa dhidi ya ukatili.

## Lengo 7: Kudumisha utambulisho wa kiutamaduni wa Taifa

Viashiria vya lengo hili bado havipo. Hata hivyo, MKUKUTA itaunga mkono taasisi na miradi ya kuelimisha ambayo inapendekeza utambulisho wakiutamaduni na umoja wa kitaifa. Lugha ya Kiswahili pia itakuzwa ndani na nje ya nchi.

# Muhtasari wa jumla ya maendeleo ya MKUKUTA mwaka wa 2006

**Kwa ujumla, maendeleo yamepatikana katika mwaka wa kwanza wa MKUKUTA, lakini vitendo zaidi vinahitajika ili kutimiza malengo katika makundi yote matatu.**

Katika **kundi I**, kasi ya ukuaji wa Tanzania inapaswa kuharakishwa. Ili kukuza kila sekta ya uchumi na sehemu zote nchi, hasa kilimo, mtazamo makini na imara unahitajika.



Kwa **kundi II**, dalili za elimu kujengeka zinaonekana, lakini lazima tuendelee kufanya kazi ili kuongeza idadi ya shule na kuendeleza ubora wa elimu. Viashiria vya afya pia vinatia moyo ingawa utaratibu wa kutoa ripoti mara kwa mara kupitia mfumo wa usimamizi wa Taarifa za afya unapaswa kuimarishwa ili hatua zote pamoja na matatizo katika afya yaweza kujulikana. Vile vile, mifumo bora inapaswa kuwekwa ili kupima juhudi za kupanua upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira katika nyumba za Watanzania wote. Kwa sababu ya umuhimu wa maji safi kwa afya bora na uzalishaji, upatikanaji wa maji safi kwa watu wote unastahili kupewa kipa umbele.



Kwa **kundi III**, huu ni mwaka wa kwanza ambapo kuna kundi la viashiria vya utawala na kuwajibika linalotumika kitaifa. Majibu ya mwanzoni yanaonyesha maendeleo kidogo lakini jitihada zinapaswa kuendelea na kuzidishwa. Jitihada nyingi zimetumika katika uchaguzi wa viashiria, lakini sehemu zingine uchaguzi ulikuwa dhaifu. Mifumo ya sera ambayo ni msingi wa viashiria vya utawala, pamoja na vile vya ulinzi wa jamii katika kundi la 2, inapaswa kuwa imara zaidi. Viungo kati ya serikali za mitaa na mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa MKUKUTA pia vinapaswa kuimarishwa.



Sehemu ya

# III Wewe na MKUKUTA

## Je, wewe unaweza kufanya nini?


**Serikali inawahimiza Watanzania wote kushiriki katika jitihada za MKUKUTA kwa:**

- Kuuchukua huu mkakati kama wao na jukumu lao,
- Kugeuza mpango, uliotengenezwa kwa ushirikiano, kuwa vitendo vya manufaa kwa nchi nzima, na
- Kusaidia kusimamia na kutathmini maendeleo ya MKUKUTA kwa hatua zilizofikiwa.

Ili MKUKUTA ufanikiwe, wananchi, jamii, viongozi wa serikali, wafanyabiashara, na mashirika ya maendeleo wote wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia shabaha za MKUKUTA.

Ukitazama elimu tu ,utaona kwamba ni watu wengi na vikundi ambao wanahitajika kufikia lengo letu la Tanzania iliyo na elimu bora:

- Wazazi wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kwamba watoto wao wote wa kiume na wa kike wanakwenda shule kila siku;
- Walimu wanapaswa kufanya bidii kuongeza elimu na ujuzi ili wafundishe wanafunzi wao vizuri;
- Viongozi wa serikali, kamati za shule zinapaswa kufanya bidii ili shule ziwe na walimu wa kutosha, madarasa, madawati, vitabu na vifaa vingine;
- Wabia wa maendeleo na mashirika mengine wanapaswa kuunga mkono miradi ya elimu; na,
- Watoto wanatakiwa kufanya bidii shuleni katika masomo yao.



## Usambazaji wa habari muhimu

**Serikali pia inahitaji taarifa sahihi kwa wakati unaofaa ili kubuni sera zitakazoleta matokeo mazuri na kuongoza shughuli za MKUKUTA ili kupunguza umaskini. Ili kufanya maamuzi sahihi wakati huu na ujao, serikali inapaswa kujua ni nini kinachoendelea katika jamii zote Tanzania.**

Hivyo basi, mfumo wa usimamizi wa MKUKUTA unataka Wizara na viongozi wa serikali kuu na za mitaa walioko sehemu zote nchini kukusanya taarifa sahihi na za wakati uliopo, na kuziwasilisha mara kwa mara katika ofisi ya uratibu. Kwa njia hii, ripoti ya MKUKUTA ya mwaka ujao itakuwa na taarifa bora zaidi kwa jamii mbali mbali kwa nchi nzima.

Kwa upande mwingine, na jamii nazo zinategemea taarifa na vitendeakazi kutoka kwa serikali ili kuweza kuendelea na shughuli za maendeleo katika mitaa yao. Hadi wakati huu, serikali imeendelea kutoa taarifa na vitendeakazi kwa jamii ili kuwasaidia kupanga shughuli zao ziwe za ufanisi na zenye matokeo yaliyotarajiwa.

Hii taarifa ya hali ni sehemu moja tu ya kutekeleza wajibu huu. Kwa kufanya hivi serikali ina matumaini kwamba itapiga hatua ya KUPUNGUZA umaskini Tanzania.

Ahsante kwa kuonyesha shauku katika MKUKUTA wa mwaka huu. Nangojea kwa hamu kuwakaribisha tena mwaka ujao. Kwaherini.



# Marejeo


Afrobarometer (2006): Briefing Paper No. 33: "Combating Corruption in Tanzania: Perception and Experience". Available at:
http://www.repoa.or.tz/documents_storage/Research%20Activities/AfrobriefNo33.pdf

Asian Development Bank (2005). Improving Technical Education and Vocational Training. Available at:
http://www.asiandevbank.org/Documents/Books/Tech_Educ_Voc_Training/macroeconomic-setting.pdf

Lindeboom, W., V. Leach, M. Mamdani, B. Kilama (2006). Vulnerable Children in Tanzania and Where They Are. March 2006. (Report submitted to UNICEF by REPOA)

Ministry of Planning, Economy and Empowerment (MPEE) (2006). MKUKUTA Monitoring Master Plan and Indicator Information. November 2006. Available at:
http://www.povertymonitoring.go.tz/documents/mkukutamasterplan.pdf

National Bureau of Statistics (2002). Household Budget Survey 2000-2001. Dar es Salaam: NBS.

National Bureau of Statistics (2003). Population and Housing Census 2002. Dar es Salaam: NBS. Available at: http://www.tanzania.go.tz/census

National Bureau of Statistics (2005). Agricultural Sample Census 2002-03. Preliminary Report of Basic Tables: Smallholder Data, 1 August 2005.

National Bureau of Statistics and Macro International (2005). Tanzania Demographic and Health Survey 2004-2005, Preliminary Report. Dar es Salaam: NBS and Macro International.

Research and Analysis Working Group (2005). Poverty and Human Development Report 2005. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers. Available at:
http://www.repoa.or.tz/documents_storage/PHDR_2005.pdf

Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS), National Bureau of Statistics (NBS), and ORC Macro (2005). Tanzania HIV/AIDS Indicator Survey 2003-04. Calverton, Maryland, USA: TACAIDS, NBS, and ORC Macro. Available at: http://tanzania.usaid.gov/documents/HIVAIDSIndicatorSurvey20032004.pdf

Tanzania Development Partners Group (DPG) (2006). The Large and Uncaptured Potential of the Forestry Sector in Developing Tanzania's Economy. Available at:
http://www.wildlife-programme.gtz.de/wildlife/download/dpgforestrybrief.pdf

Vice-President's Office (VPO) (2005). National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (NSGRP). June 2005. Available at: http://www.povertymonitoring.go.tz/documents/mkukuta_main_eng.pdf

World Bank (2005). Study on Growth and Environmental Links for Preparation of Country Economic Memorandum, Part 1. May 2005. Available at:
http://easternarc.or.tz/downloads/General/CMEAMF/Economics/WB_CEM_05/MAIN_REPORT_Part_1_final.pdf

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| **ARV** | Dawa za Kupunguza Makali ya Ukimwi |
| **GDP** | Pato la Taifa |
| **HBS** | Utafiti wa Bajeti ya Kaya |
| **ILO** | Shirika la Kazi Duniani |
| **MDAs** | Wizara, Idara na Wakala wa Serikali |
| **MMEM** | Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi |
| **MKUKUTA** | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| **MW** | Megawatti |
| **NBS** | Kitengo cha Takwimu za Taifa |
| **PMO-RALG** | Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TAMISEMI** | Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa |
| **TDHS** | Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya wa Tanzania |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |